

AHMAD DABBAGH

MKUU WA CHUO CHA UINGEREZA CHA SAYANSI YA
KIISLAMU NA MKURUGENZI WA CHUO CHA WISELIFE


zawiyah.org

prophetic-path.com

facebook.com/ShaykhAhmadDabbagh



Swahili



YALIYOMO

2

Wasifu

Historia, masomo na sifa za ustahili

5

Nchi alizozuru

Nchi mbalimbali alizozuru kuendeleza shughuli iliobarikiwa ya Da'wa

6

Mikutano

Orodha ya mikutano mbalimbali alizohudhuria

8

Maelezo ya jumla ya taasisi

Mtazamo mfupi wa taasisi mbalimbali zinazo ongozwa na Ahmad Dabbagh

9

Njia ya Muhammadiyah

Muhtasari wa njia ya kujitakasa inayobadilisha maisha

10

Chuo cha Wiselife

Mitaala mbalimbali mifupi ya kijuzi ya kusaidia katika changamoto za maisha kama ndoa

12

Shirika la Dabbagh la ustawi wa kijamii

Tawi la hisani la Tareeqah Muhammadiyah

13

Chuo cha sayansi ya kiislamu cha Uingereza

Mitaala zinazorahisisha upatikanaji wa masomo muhimu ya kiislamu

14

Kufunua visivyoonekana

Mapumziko yaliyoundwa kufundisha watu kuona na kupata uzoefu wa ulimwengu wa visivyoonekana

16

Ushauri na mafunzo

Kutoa ushauri wa dhati na mwongozo kwa watu

17

Vipindi vya uponyaji bila malipo

Huduma ya bure yenye malengo ya kutibu magonjwa ya kimwili, kiakili na ya majini kutumia mafunzo ya kinabii

18

Vitabu vilivyoandikwa na Ahmad Dabbagh

WASIFU



ASILI YA FAMILIA

Imam Hassan al Basri رحمه الله عليه alikuwa miongoni mwa wasomi wakubwa na mcha mungu katika kipindi cha Tabi'een aliyejifunza dini na kuandamana na maswaha-ba wakubwa wa mtume صلى الله عليه وسلم . Mmoja wa wazao wake aliamia Kashmir ili kufikisha ujumbe wa kiislamu. Hapo aliandamana na Shaykh Bhaudeen Zakariyah Multani Suharwardi رحمه الله عليه ambaye aliwaambia wahamie mahali ilio karibu na Kharjan, Gujarat katika mkoa wa Punjab. Jina lake lilikuwa Shaykh Khayru-deen Auliyah رحمه الله عليه na aliipa hiyo mahali jina la "Haqeeqah" kumaanisha " Ukweli " . Walieneza ujumbe wa kiislamu katika karne ya 8 kwenye maeneo hayo na mamia ya watu waliingia dini ya kiislamu kwa mikono yao. Ahmad Dabbagh ni mzao wao na alizaliwa katika kijiji kilicho karibu na Sumandr, Pakistan. Alihamia nchi ya Denmark akiwa na umri wa miaka 5 na kuanza masomo ya chekechea katika mji uitwao Ishoj nchini Denmark.

ELIMU YA MSINGI

Akiwa na umri wa miaka 6 na baada ya kumaliza masomo ya Quran , alianza kuihifadhi Quran. Miaka 7 iliofuata aliitumia kusoma sayansi ya kiislamu. Baada ya hapo alitumia miaka kadhaa kusomea Pakistan na Uingereza. Alisafiri pia kuenda Iraq, Syria na Moroko. Ahmad Dabbagh hasemi kuwa yeye ni msomi ila ana ruhusa kadhaa kufunza sayansi mbalimbali ya kiislamu kama vile Tafseer, Hadith, Fiqh na Tazkiyah. Amean-dika vitabu kadhaa katika maudhui anuwai na zinapatikana kwa lugha nyingi.

ELIMU YA KISEKULA

Katika elimu ya kisekula, alisoma hadi kiwango cha uzamili katika chuo cha Salford, Manchester na MBA (shahada ya uzamili katika usimamizi wa biashara) katika chuo cha Central Lancashire. Alifanya kazi kwenye viwanja mbalimbali kama uhasibu,uuzaji,huduma ya majela na pia alipata mafunzo ya kufanya kazi kwa idara ya polisi.

VYUO VYA ELIMU

Kwa miaka kadhaa zilizopita alianzisha vyuo anuwai, vikundi vya utafiti , vikundi vya dhikr , vyuo vikuu na vyuo vya elimu katika nchi za Uingereza, Denmark, Pakistan, Canada, Bangladesh, Marekani na Moroko.

HUDUMA ZA KIBINADAMU

Ahmad Dabbagh analenga utakasaji wa nafsi na kujiendeleza kibinafsi ili mtu aweze kutakaswa kutoka mawazo hasi, matendo, hisia , vitendo na maadili mabaya kwa kuzibadilisha na mawazo chanya, matendo, hisia ,vitendo na maadili mema.Njia hii inajulikana kama njia ya kinabii (Tareeqah Muhammadiyah) . Baada ya hapo watu hao hupelekwa kwenye kiwango cha mwanga , ambapo baada ya hapo mtu huwa na mahusiano bora kabisa na mungu na viumbe vyake.

Njia hii ya utakasaji inatokana na Qur'an ,Sunnah , maelezo ya Ahl ul Bayt, maswaha kama Sayiduna Ali bin Abi Talib رضي الله عنه , Sayiduna Imam Hassan, Imam Hussayn رضي الله عنه , Imam Zainulabideen رضي الله عن , imam Hasan Basri , Sayiduna Abdul Qadir al-Jilani , Sayiduna Imam Abul Hassan Shadhili رضي الله عنه na mcha mungu mkubwa wa zama za banii Umayyah, Sayiduna Abdul Azeez Dabbagh رحمه الله Ana ijaza ya madhehebu ya Qadiriyah, Shadhiliyah, Rifaiyah, Suharwardiyah, Chistiyah na Naqshbandiyah

SAFARI ZAKE

Ahmad Dabbagh anasafiri sana kwa miezi 7 kwa mwaka, kutoka Canada hadi mashariki ya mbali kama Malaysia na Indonesia , na kuongea na wote kutoka wanakijiji maskini hadi Wataalamu wa vyo vikiu na maafisa wa serikali.

SHUGHULI ZA MISAADA

Ili kusaidia wasiojiweza kifedha au kimwili , ameanzisha Dabbagh Welfare Trust inayosaidia mafukara katika nchi nyingi.

IMANI NA MADHEHEBU ZAKE

Yeye ni wa Ahlus-Suunah wal Jama'ah na anapenda sana Ahlul Bayt . Anafuata Fiqh ya Hanafi na kuheshimu ma Imam wengine . Anafuata njia ya ma Auliyah na wacha mungu na kufuata vizuri Shariah na Sunnah.

MAISHA YA KIFAMILIA

Ameoa na anaishi na mkewe na watoto wake mjini Manchester, Uingereza



ELIMU



ELIMU YA KIISLAMU

1975-1989 Aqeedah :
Sanad kufikia Imam Abu Matureedi رحمه الله

Fiqh : Sanad kufikia Imam Abu Haneefah رحمه الله

Hadith : Ijazah kwa vitabu sita vya Hadith,
Saheeh Bukhari Muslim, Abu Dawood, Nisa'ie,
Tirmidhi na Ibne Majah

Tazkiyah : sanad kufikia Syaiduna Abdul Qadir Al Jilani رحمه الله

Seerah, misingi ya Dini na Sanad ya Hifz ya
Quran nzima.

ELIMU YA KISEKULA

MBA na DBA

1990-1995
Chuo kikuu cha Salford na Chuo cha Central Lancashire

BTEC Diploma ya kwanza katika biashara na Uhasibu

BTEC Diploma ya kitaifa katika biashara na Uhasibu


Shahada ya uzamili katika usimamizi wa biashara

Diploma ya DPSI katika kutafsiri huduma za umma

1995 hadi Leo vyuo mbalimbali

Kufunza lugha (Kiingereza, Urdu, Kiarabu)

NCHI ALIZOZIZURU



MIKUTANO ALIZOHUDHURIA



Mkutano wa kimataifa wa Sufi ,Fez, Moroko

Mkutano wa kiislamu wa kimataifa wa kiroho, Toubia, Senegal



Maisha na mafunzo ya Imam Zain Al-Abidin – Iraq

Mkutano wa kimataifa wa walimu, Lahore, Pakistan



MIKUTANO ALIZOHUDHURIA

Mkutano wa ulimwengu wa Shahada, Malaysia



Mkutano wa kimataifa , Indonesia



Mkutano wa Sunni , Uingereza



Mkutano wa kimataifa , Uturuki



Pia alihudhuria:
Chuo kikuu cha Yale, Marekani
Chuo kikuu cha Manchester, Uingereza



Tareeqah Muhammadiyah

Mtaala wa kijuji katika utakasaji nafsi

PROGRAMU YA KUPANDA WEO KATIKA SEKTA YA KIROHO

Kufika kiwango cha Haqul Yaqeen
kupitia swala na maombi



CHUO CHA WISELIFE
Programu ya kibunifu na kijuji ya kutatua
changamoto za kila siku kote duniani



CHUO CHA UINGEREZA CHA

SAYANSI YA KIISLAMU

Uwanja wa kuwezesha kujifunza
elimu ya kimsingi ya kiislamu




**PROGRAMU YA
MATIBABU YA BURE**
Huduma za Ruqya na matibabu ya
bure kulingana na Qur'an na Sunnah

SHIRIKA LA DABBAGH LA USTAWI WA KIJAMII

Kusaidia mafukara kote ulimwenguni

TAREEQAH MUHAMMADIYAH



Allah mtukufu amemtuma mtume صلى الله عليه وسلم ili awafunze wanadamu jinsi ya kutumia umri wao kumuabudu Allah, ili kumridhisha. Tareeqah Muhammadiyah ni njia ya utakasaji nafsi inayomsaidia mtu kufikia lengo hili.

Ili kumridhisha Allah, mja anfaa kuwa na sifa zifuatazo :

1. Kumpa Allah ﷻ kipaumbele
2. Kumpa mtume صلى الله عليه وسلم kipaumbele
3. Kuwaonyesha viumbe huruma
4. Kujua kila mara kuwa mungu anakuona

1.UTAKASAJI WA MWILI

Ili kulinda viungo kutokana na madhambi za ulimi, masikio, macho, mikono, miguu, tumbo na sehemu za siri.

2.UTAKASAJI WA AKILI

Kulinda moyo na ubongo kutokana na mawazo mabovu, na kuyabadilisha na mawazo mema mazuri na kuweka kwa akili uwepo wa Allah kila mara.

3.UTAKASAJI WA MOYO NA ROHO

Kuondoa kabisa tabia chafu kama husuda, chuki, kujionyesha na kiburi zinazokuwa moyoni, kisha kurembesha nafsi na tabia nzuri kama ukweli, subra, shukrani, uaminifu na kujiepusha na mabaya

4.KUANGAZA ROHO

Kuelekeza ndani na nje katika upande wa upendo wa Allah na mtume صلى الله عليه وسلم ambapo matokeo itakuwa kupata radhi za Allah na kuwa karibu naye.

Baada ya kumaliza viwango vinne vya utakasaji, undani wa mja utapata mwanga kutokana na ushuba na upendo wa Allah, na atanza kuita wengine kuchukua njia aliochukua yeye.

CHUO CHA WISELIFE



Mkurugenzi mkuu : Ahmad Dabbagh

TAMKO LA LENGU :

Kueneza mwanga wa hekima ya mungu na ya kibinadamu kwa njia ya kijuzi inayofaa na yenye maana katika maisha ya kila siku , na kutatua changamoto za kila siku kote duniani.

KUHUSU

Kama waislamu wenye umri mdogo, tunaishi katika wakati ambapo wanadamu wanapata elimu ya kiwango cha juu na taarifa na habari kushinda wakati mwingine wowote.Hata hivyo,ingawa kuta zetu zimepambwa na shahada mbalimbali na akili zetu zimejaa taarifa , kuna uwezekano sisi sio kizazi chenye hekima zaidi kuliko vizazi vyote vilivyowahi kuishi.Haimaanishi kuwa kizazi chetu hakina hekima, bali ni kuwa tumepoteza uzingativu; na kushindwa kuchuja taarifa zote hizo tunazozipata ili kupata maisha bora na yenye natija.



WALICHOKIFANYA MPAKA SASA

Chuo cha Wiselife imepanga semina kwa Uingereza,Marekani,Denmark na Pakistan ambapo zaidi ya watu 500 wamehudhuria. Wiselife imefaulu kupata kiwango cha mapendekezo cha 100% kutoka waliohudhuria kupendekeza chuo cha Wiselife kwa familia na marafiki.



SEMINA

IMARISHA NDOA YAKO

Imarisha Ndoa Yako inatokana na misingi ya kiislamu ila imeundwa kuwa hudumia wanandoa wote na wanaotafuta kuoa, wenye msingi wa kiislamu na wasiokuwa nao. Semina hii inashughulikia maudhui za kimwili na kiakili za ndoa. Gundua uhalisia wa mapenzi, gundua aina ya utu wako inayofunzwa kulingana na misingi ya Quran na Sunnah ikichanganywa na mbinu za sayansi ya kisasa na saikolojia.

KUFUNGA; ZAIDI YA NJAA NA KIU

Ramadan sio tu kukaa njaa, ni fursa ya kubadilisha maisha na kuungana kiroho. semina hii inashughulikia maudhui kama kuongeza utashi, kukuza umakini, kukuza utumiaji mzuri wa wakati na kukuza upande wa kiroho.

“kutatua changamoto za kila siku, kote duniani”

SEMINA ZIJAZO:

- UHURU KUTOKA URAIBU
- UGUNDUZI WA MAISHA
- KUKABILIANA NA MSIBA

IMARISHA TABIA YAKO

Semina ya siku mbili ya kuimarisha tabia, ilio na misingi ya kiislamu. Inajumuisha njia za kipekee ili kuelewa jinsi unaweza kubadilisha tabia hasi na kukuwa na tabia inayoonyesha mazuri ya ubindamu. Semina hii inashughulikia maudhui za tabia nzuri, kudhibiti hisia, kusafisha moyo na njia ya tabia mbaya.



ASILIMIA 100% YA WASHIRIKI WANGEPENDEKEZA CHUO CHA WISELIFE KWA MARAFIKI NA FAMILIA



dabbaghwelfare.org.uk

SHIRIKA LA DABBAGH LA USTAWI WA KIJAMII



Mfadhili- Ahmad Dabbagh

TAMKO LA LENGU

Kutumikia ubinadamu kwa kujitolea kushughulikia mafukara katika jamii ya wanadamu, kuanzia watu binafsi, familia, mayatima na jamii kutimiza mahitaji yao ya kila siku.

KUHUSU

Dabbagh Welfare Trust ina lengo la kusaidia watu maskini kabisa duniani kote katika misiba yao, kwa kusambaza sadaqah, Zakat na Lillah kwa njia ya kinabii. Pia ina lengo la kusaidia watu wakati wa majanga na dhuru, ni shirika huru lisilo la kiserikali lililoanzishwa Uingereza mwaka wa 2011. Dabbagh Welfare Trust inasambaza pesa zilizokusanywa kwa kupitia mfumo wa kupeleka ombi kwa shirika, na kupitia mawakili walioko sehemu tofauti tofauti, na hili hurahisishia wafadhili kuchagua mahali ambapo wanataka pesa zao zigawanywe bila ubaguzi.

VITU WALIVYOVIFANYA

Wamepeleka msaada Uingereza, Pakistan, India, Bangladesh, Myanmar, Syria, Philippines, Gaza, Tanzania n.k. Katika miradi tofauti kama vifurushi vya chakula, ndoa za pamoja, visima, usafishaji wa maji, matibabu ya macho, elimu, zawadi kwa watoto, pakiti za msimu wa baridi, usaidizi wakati wa majanga, uzalishaji wa mapato, huduma kwa mayatima, da'wa na makao.



Asilimia
95% ya
michango
huwafikia
wahitaji.



CHUO CHA SAYANSI YA KIISLAMU CHA UINGEREZA



Mkurugenzi- Ahmad Dabbagh

TAMKO LA LENGU

Kueneza mafunzo ya Ahlus Sunnah Wal Jamaa kwa mfumo uliopangwa vizuri na kuwezesha watu wa aina zote kupata elimu.

Lengu la Ja'amia Muhammadiyah ni kuwezesha upataji wa elimu muhimu ya sayansi ya kiislamu kama vile imani (Aqeedah) , Sheria ya kiislamu (Fiqh) , Usomaji wa Qura'n (Tajweed) na utakasaji(Tazkiyah) na sayansi nyingine nyingi. Ingawa Ja'amia Muhammadiyah inashughulikia vizuri mada zote za kiislamu, uwanja wetu mkubwa ni Da'wah (kueneza uislamu) na Tazkiyah . Ja'amia Muhammadiyah inaamini kuwa kando na Ta'leem (elimu) kuna haja ya kushughulikia kwa ndani upande wa vitendo katika elimu ya kiislamu (Tarbiyah) . Elimu (ilm) pekee haitakuwa inatosha mpka elimu hii iwekwe kwenye vitendo.

Ja'amia Muhammadiyah imeanzisha vituo katika sehemu za Bolton, Hyde, Oldham, Manchester, Eccles ,Birmingham, London, Denmark ,Marekani na Pakistan

Programu kadhaa za kielimu zinatolewa katika viwango tofauti ili kuwezesha watu wa umri tofauti kupata elimu. Ikiwa unatafuta kusasisha elimu ulionao au unatafuta programu yenye mpangilio ukiwa kwenye njia yako ya kuwa Alim au Alimah mwenye ujuzi, ni hakika kuwa tunao programu inayotimiza mahitaji yako.

Tuko na mitaala zifuatazo : Mitaala fupi za Aqeedah, Fiqh, Usool Fiqh, na Tazkiyah

Semina zinazoshughulikia mada nyingi tofauti kama vile :

Utumiaji mzuri wa wakati, uangalifu, kukabiliana na changamoto za ndoa, uchawi, maudhui za kiroho na madarasa ya uchumi wa nyumbani.

KUFICHUA VISIVYOONEKANA



Wanadamu daima walikuwa wakitafuta ukweli na uhalisia. Kwa ulimwengu ulioshuhudia maendeleo makubwa ya kiteknolojia na kisayansi, kumekuwa na kukatika kwa mahusiano kati ya ulimwengu wa vinavyoonekana na visivyoonekana, na kwa hiyo sababu wengi wameanza kujiuliza uwepo wa ulimwengu usioonekana, yaani Ahera. Ingawa jamii nyingi zinaamini ulimwengu usioonekana kwa sababu ya vitabu vyao, uwepo wa imani hii katika kutafuta maisha chanya yenye maana na malengo umepotea pole pole.

Hili limetufanya mara nyingi kutimiza lengo hilo kupitia njia zenye uharibifu. Limetufanya tujitenge na umati tukihisi majonzi na daima tukitafuta matimizo ya mahitaji yetu ya kiroho bila kufaulu. Ili kukumbana na changamoto hizi, mapumziko yameundwa ili kuwapa washiriki hisia ya ulimwengu usioonekana, na kujenga viwango vitatu vya imani vilivyotajwa hapo chini.

Mapumziko haya hukuza mahitaji ya kiroho ya binadamu kwa njia ya kisheria, na kusasisha mahusiano baina ya washiriki na Allah جل جلاله na kuwaunganisha washiriki na malengo makuu ya maisha.

VIWANGO VITATU VYA IMANI

1. 'Ilm ul Yaqeen (Elimu ya imani)
"Elimu ya Uhakika"(102:5)
2. 'Ayn ul Yaqeen (Kuamini unachokiona)
"jicho la ukweli"(102:7)
3. Haqq ul Yaqeen (uzoefu wa imani)
"Ukweli wa uhakika" (56:95)



AINA TOFAUTI ZA MURAQABAH (TAFAKURI)

Muraqabah e Miraj – Kuingia ulimwengu wa kiroho na kushiriki katika safari ya kiroho kuenda Fez, Madinah Munawwarah, Makkah al Mukarrama, Masjid al Aqsa , mbingu 7, maisha ya Barzakh, mti wa Lot na zaidi ili kukuza imani ya visivyoonekana na kupata mwelekezo ili kuleta imani hii kwenye vitendo vyetu.

Muraqabah e Barzakh- Kuingia ulimwengu wa kiroho kuona maisha ya Barzakh (kaburi) ili kuweka taswira ya kaburi kwenye akili. Washiriki wanapata kujua maisha ya Barzakh , ili kukuza imani na hili litawawezesha kufuata Shariah vilivyo.

Muraqabah e Muhammadiyah – Kuingia ulimwengu wa kiroho na kushuhudia uwepo wa Mtume صلى الله عليه وسلم . Washiriki wanapitia viwango kadhaa, ambapo katika kiwango cha mwisho watashuhudia uwepo wa mtu bora kabisa ulimwenguni , Sayyiduna Muhammad صلى الله عليه وسلم.

Muraqabah e Dua – kujiunga na Allah جل جلاله na kuwa katika uwepo wa Allah جل جلاله kwa mwili, akili, moyo na roho, ili kuwa na uhusiano mzuri na kuomba Allah جل جلاله anisamehee madhambi zangu , na kumshukuru kwa neema zake , na kuleta kwa uwepo wake mahitaji yangu na wasiwasi wangu, na kumuomba mwongozo katika maisha yangu na kisha kumtegemea Allah جل جلاله kwa matokeo.

Muraqabah hizi zinafunzwa kwa mapumziko ya siku 2-4, ambapo mshiriki anatolewa kutoka kiwango cha ulimwengu ili aweze kuhisi ulimwengu wa visivyoonekana. Washiriki wanatoka tabaka tofauti katika jamii, kutoka wanakijiji hadi wataalamu wa vyuo vikuu.



USHAURI NA NASAHA



Mwalimu wa Tareeqah Muhammadiyah, Ahmad Dabbagh antoa kikao huru cha ushauri wa bure katika mazingira ya siri, akisikiza watu kwa makini na kuwapa wakati wake, huruma zake, elimu yake na heshima zake kwa wanaozihitaji.

Lengo lake kuu ni kutoa huduma ya bure ili kuwezesha watu kufikia malengo yao ya maisha, na kupeana ushauri wenye ubunifu, ujuzi na usasa inayochanganya mafunzo ya kinabii na sayansi ya kisasa.



Kutokana na uzoefu wake pana na hekima yake katika sekta ya kiislamu na kisekula, anapeana ushauri, na maelekezo kwa wanaozihitaji. Hii inatokana na pande zote za maisha kama kibinafsi, kijamii, kielimu, kiislamu, kifamilia, kiroho na majukumu ya kiutawala ya taasisi wanazoziongoza.

Huduma isiyo na ubinafsi ya mwalimu imesaidia maelfu ya watu wapate ushujaa katika viwanja mbalimbali vya maisha yao, ambayo imesababisha umaarufu nchini na ulimwenguni, na foleni zinachukua sehemu kubwa ya usiku. Watu wengi kutoka nchi mbalimbali wanamkuja ili kufaidika na vikao vyake vya nasaha na ushauri, kwa mfano Uingereza, Pakistan, Malaysia, Indonesia, Moroko, Denmark, Canada, Marekani na kadhalika, ili kupata nasaha kuhusiana na changamoto mbali mbali. Hili linaonyesha huduma kubwa anaoutoa kote duniani.

Vikao vya bure vya nasaha na ushauri havitegemei wakati na mahali, kwani yeye hujibu kila mara barua pepe, na pia simu na ujumbe. Wakati anaposafiri na kueneza mafunzo ya kinabii duniani, anatoa ushauri na nasaha za kubadilisha maisha katika wakati wake wa kupumzika.

VIKAO VYA BURE VYA UPONYAJI




Vikao vya bure vya uponyaji vya pamoja vina lengo la kutoa huduma, ambapo magonjwa ya kimwili, kiakili au kiroho yanatibiwa kutumia mafunzo ya kinabii.

Changamoto zinazo wakabili wanadamu kama magonjwa zinafanya watu binafsi, familia na wapendwa wahisi kulemewa na kukosa matumaini. Kutokana na hisia za kupindukia, watu mara nyingi hutafuta suluhisho kila mahali, - na mara mara suluhisho hizo hukiuka shariah.



Vikao vya uponyaji vinaziba masafa na kupeana huduma ambapo washiriki wanaohisi kuwa wamelemewa kabisa wanapewa msaada ya kimatendo na kiroho ili shida zao ziwaondokee. Tunategemea Allah جل جلاله pekee kwani kati ya sifa zake zisizoisha ni 'Ash Shafi' (Anay-etibu).

Magonjwa huwa na sifa ya uoekee ambapo kila mshiriki ana ugonjwa wake tofauti na wengine, kwa hivyo wanatoa vikao vya moja kwa moja ili kushughulikia watu wanaotaka kusema

Shida zao kwa mazingira ya kisiri. Pia, hii inalingana na Shariah, ambapo wanawake wanafaa kuja na Mahram wao, la sivyoo hawatashughulikiwa.



VITABU ALIVYOVIANDIKA AHMAD DABBAGH



Safari ya kupata Radhi na ukaribu wa Allah جل جلاله inayopatikana kwa lugha nyingi kama Kiarabu, Urdu, Kituruki, Kifaransa, Malay, Danish, Bangla, Kiitaliano.

Vitabu vyote vilivyoandikwa na Ahmad Dabbagh vinatafsiriwa kwa lugha nyingi iwezekanavyo, ili dunia nzima ifaidike.



AHMAD DABBAGH

MKUU WA CHUO CHA UINGEREZA CHA SAYANSI
YA KIISLAMU NA MKURUGENZI WA CHUO CHA WISELIFE

zawiyah.org
prophetic-path.com
facebook.com/ShaykhAhmadDabbagh
